

- (vii) Laini ya Lessos – Tororo (Kilomita 132.5, 400kV) (Mradi wa Kuunganisha Kenya-Uganda);
- (viii) Laini ya Machakos – Konza – Kajiado – Namanga (Kilomita 107, 132kV);
- (ix) Laini ya Turkwel – Ortum – Kitale (Kilomita 90, 220kV; na
- (x) Laini ya Menengai – Soilo (Kilomita 13, 132kV).
- (xi) Laini ya Loiyangalani – Suswa (Kilomita 430, 400kV);
- (xii) Laini ya Olkaria – Lessos – Kisumu (Kilomita 300, 400/220kV) ya saketi mbili na kazi za ujenzi wa kituo kidogo cha umeme huko Olkaria, Lessos na Kisumu; na
- (xiii) Barabara Kuu ya Umeme ya Afrika Mashariki (Kilomita 12, 500kV HVDC (Mradi wa Kuunganisha nchi za Ethiopia–Kenya) laini yenye uwezo wa kusafirisha umeme kwa njia ya bipolar yenye kituo kidogo cha kubadilisha umeme wa DC/AC na kituo kidogo cha umeme chenye nguvu ya 400/220kV.

Mchakato wa kupata washauri na wahandisi wa EPC kwa miradi ifuatayo umekamilika:

- (i) Laini ya Lamu – Kitui – Nairobi Mashariki ya saketi mbili (400kV kilomita 520);
- (ii) Kituo kidogo cha umeme cha Mariakani 400/220 kV
- (iii) Mradi wa kuunganisha Kenya – Tanzania (400kV ya kilomita)

Kampuni inaendelea kutafuta ufadhili kwa ajili ya miradi ifuatayo ya Megawati 500+, na shughuli za awali kama vile uthamini wa ESIA na RAP na mchakato wa kutafuta washauri wasimamizi zime-shafanywa:

- (i) Laini ya Menengai – Rongai (Kilomita 25, 400kV)
- (ii) Laini ya Silali – Rongai (Kilomita 150, 400kV)

- (iii) Laini ya Isinya – Nairobi Mashariki (Kilomita 110, 400kV)

Kampuni imekamilisha uchambuzi yakinifu wa miradi mipya 36 ya laini za kusambaza umeme kwa ngazi mbalimbali za msongo wa umeme nchi nzima kwa ajili ya uwekezaji wa baadae, fedha zinazohitajika kutekeleza miradi hii ni takribani Dola za Marekani Bilioni 2.1.

Miradi iliyo chini ya utekelezaji iko kwenye vipengele vinne vya jumla kulingana na malengo husika, yaani:

- i. Miradi ya Kuimarisha Mfumo;
- ii. Miradi ya Kusafirisha Umeme kutoka Vituo vya Kuzalisha Umeme;
- iii. Miradi ya Kuunganisha nchi za Ukanda; na
- iv. Miradi ya Upatikanaji wa Umeme.

Maelezo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoendelea ya kusambaza umeme yametolewa hapa chini: -

I. Miradi ya Kuimarisha Mfumo

Miradi ya kuimarisha mfumo/kuongeza uwezo itaboresha uwezo wa kusafirisha nishati ya umeme na kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa nguvu ya umeme, hasara kubwa inayopatikana wakati wa kusambaza umeme, kukosekana kwa uhakika wa ugavi na usalama wa mtandao. Miradi hiyo ni pamoja na:-

Laini ya Kusambaza Umeme ya Mombasa–Nairobi (220 kV, Kilomita 482)

Hii ni laini ya kilomita 482 yenye uwezo wa 220kV na saketi mbili kutoka kituo kidogo cha umeme cha Rabai hadi Embakasi na ina uwezo wa kubeba nguvu ya umeme wa Megawati 1500. Mradi unalenga kuziba pengo kati ya usambazaji wa nguvu katika Mkoa wa Pwani kwa ajili ya kusambaza katika vituo vya uhitaji zaidi jijini Nairobi na maeneo







Ufungaji wa
nyaya za umeme
kwenye mradi
wa Mombasa-
Nairobi


<<<<<<<<<<<<

Ujenzi wa kituo kidogo cha umeme cha Suswa ulikamilika kwa asilimia 100 katika mwaka huu. Mafaniko mengine yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa misingi ya minara, kusimamisha minara na kuweka nyaya. Kazi ya Ukandarasi katika vituo vidogo vya umeme vya Athi River, Isinya and Kimuka zilisimamishwa kutokana na kusitishwa kwa mkataba wa kandarasi wa “EPC contractor” na utaratibu wa kutafuta mkandarasi mpya ulianza. Laini ya Suswa-Isinya inatarajiwa kuanza kutumika mwezi Desemba 2016. Ujenzi wa jumla wa kituo kidogo cha umeme cha Isinya umekamilika kwa asilimia 91. Ujenzi wa jumla wa kituo kidogo cha umeme cha Athi River umekamilika kwa asilimia 72.5, ujenzi wa jumla wa kituo kidogo cha umeme cha Kimuka umekamilika kwa asilimia 64.5 huku vifaa vya kituo kidogo cha umeme cha Komarock vimeshanunuliwa. Vituo vidogo vya umeme vya Athi River na Isinya vitakamilika mwezi Machi 2017 huku vya Kimuka na Komarock vitakamilika ifikapo mwezi Desemba 2017.

Laini ya Olkaria – Lessos – Kisumu (Kilomita 300, 220/400kV)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya kusambaza umeme ya saketi mbili ya 400kV yenye urefu wa kilomita 300 kutoka mtambo wa umeme wa jotoardhi wa Olkaria hadi Lessos, laini ya saketi mbili ya 220kV kutoka Lessos hadi Kisumu, kituo kidogo kipya cha umeme cha 200kV Kisumu na upanuzi wa vituo vidogo vya umeme vya Olkaria na Lessos (Olkaria-Lessos vikiwa na uwezo wa Megawati 1200 na Lessos- Kisumu vikiwa na uwezo wa Megawati 500). Mradi wa Olkaria-Lessos-Kisumu utasaidia kuimarisha kiungo kati ya South Rift ambapo kuna fursa kubwa ya umeme wa jotoardhi na sehemu za magharibi mwa gridi ambapo uhitaji unakua kwa kasi. Kwa kuongezwa uwezo wa kituo kidogo cha umeme cha Lessos, kitaweza kutoa kiungo madhubuti cha usambazi wa nje/ndani/kutoka nchi za jirani.

Mradi huu unadhaminiwa na JICA na Serikali ya Kenya kwa jumla ya gharama za KSh. Billioni 13.2 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Machi 2018. Katika mwaka wa ukaguzi mchoro wa ki-handisi na fidia kwa ajili ya malipo ya ufinyu wa njia



>>>>>>>>>>>>>



Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya 400kV na saketi mbili zenye urefu wa kilomita 430 ambayo itasafirisha umeme kutoka katika kituo cha kuzalisha Nishati ya Upepo wa Megawati 300 wa Ziwa Turkana huko Loiyangalani hadi kituo kidogo cha umeme cha Suswa. Kwa nguvu ya kusafirisha umeme ya Megawati 1300, laini hii itakuwa na uwezo wa kutosha wa kusafirisha umeme kutoka katika vituo vya kuzalisha umeme vitakavyowekwa kwenye uwanda wa jotoardhi katika Bonde la Ufa na mashamba ya upepo huko Mashariki ya Kenya



(Marsabit).

Jumla ya gharama za laini hii ni KSh. Bilioni 16.5 na imedhaminiwa na Serikali ya Uspeni kwa KSh. Bilioni 12 na Serikali ya Kenya kwa KSh. Bilioni 4.5. Katika mwaka tuliokuwa chini ya ukaguzi ujenzi wa laini na vituo vidogo husika vya umeme pamoja na haki ya umiliki ulipiga hatua kubwa. Kazi na vifaa vya uhandisi katika kituo kidogo cha umeme cha Loiyangalani ulianza, ujengaji wa msingi wa mnara wa 225/988 ulikamilika na minara 21/988 ilisimamishwa. Ukamilifu wa mradi huu na ufunguzi wake unatarajiwa kufikia mwezi Aprili 2017.

Laini ya Olkaria – Suswa (Kilomita 25, 220kV)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini yenye uwezo wa 220 kV na saketi mbili iliyo na urefu wa kilomita 25 kutoka mtambo wa umeme wa Megawati 280 wa Olkaria IV na Kipengele kimoja cha zia-da ya mtambo wa jotoardhi hadi kituo kidogo cha umeme cha Suswa. Uwezo wa pamoja wa laini hizi ni Megawati 1000 na umefadhiliwa na JICA, AFD, EIB na Serikali ya Kenya kwa gharama ya KSh. Bilioni 0.9. Mkandarasi wa laini hii ni KEC International (India) pamoja na SKM kama washauri uhandisi. Mradi huu umetekelezwa na KenGen. Ujenzi wa laini za kusambaza umeme umefikia ukamilifu wa asilimia 98.85 na unatarajiwa kufunguliwa mwezi Septemba 2016.

Miradi iliyo chini ya uzalishaji wa haraka wa Megawati 5,000+

Miradi iliyopo katika programu hii inalenga kusafirisha ugavi wa ziada wa umeme iliyo chini ya miradi ya Megawati 5,000+. Mradi mmoja mmoja umeainishwa hapo chini:-

a) Laini ya Menengai – Soilo (Kilomita 13, 132kV)

Mradi huu ni wa laini ya 132kV na saketi mbili iliyo na urefu wa kilomita 13 na kituo kidogo cha umeme cha 220/132kV –200MVA cha Soilo. Mradi huu unafadhiliwa kikamilifu na Serikali kwa makadirio ya gharama za KSh Bilioni 0.8. Pindi

utakapokamilika, mradi huu utatoa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Mtambo wa Jotoardhi wa Menengai wa Megawati 90. Ukamilifu wa jumla wa mradi huu umefikia asilimia 92, huku kituo kidogo cha umeme kikiwa katika hatua ya kufanyiwa majaribio. Mradi huu ulikamilika mwezi wa Desemba 2016.

b) Laini ya Menengai – Rongai (Kilomita 30, 400kV)

Mradi huu unajuhumisha laini ya 400kV na saketi mbili na vituo vya umeme vya vyenye uwezo wa 400/220kV – 200MVA vya Menengai na Rongai. Mradi unalenga kusafirisha umeme kutoka




Mkurugenzi Mkuu wa KETRACO (kati) na waafanyikazi wake wakizuru kituo cha umeme huko Loiyangalani

<<<<<<<

>>>>>>>>>>>>>



Ili kuwezesha biashara ya umeme katika ukan-
da huu, KETRACO imeendelea kushirikiana na
mashirika ya kikanda ya nishati ya umeme katika
ari ya ushirikiano wa kiuchumi. Ili kukuza uhusi-
ano wa kikanda wa nishati ya umeme, Kampuni
inatekeleza miradi ifuatayo ya umeme ya kuungan-



isha nchi za jirani:

Laini ya kusambaza umeme ya Lessos-Tororo (Kilomita 127, 400kV Kuunganisha Kenya-Uganda)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya kilomita 127 ya uwezo wa 400 kV ya saketi mbili kutoka kituo kidogo cha umeme cha Lessos nchini Kenya hadi Tororo nchini Uganda yenye uwezo wa kufafirisha umeme wenye nguvu ya Megawati 1200. Mradi huu ni sehemu ya mtandao wa nishati ya umeme ambao utaunganisha Kenya na Uganda, Rwanda, Burundi na sehemu ya Mashariki ya Congo (DRC) chini ya programu ya kikanda ya Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Program (NEL-SAP) na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) na Serikali ya Kenya kwa gharama ya KSh. Bilioni 4.9. Utatoa uwanda kwa ajili ya biashara ya nishati ya umeme mbali na kuwezesha umadhubuti wa gridi katika ukanda huu.

Shughuli za ujenzi wa kituo kidogo cha umeme cha Lessos, kujenga misingi ya mnara na usimamishaji wake ziliendelea katika kipindi tulipokuwa chini ya ukaguzi, lakini zikasimama hapo baadae kutokana na kusitishwa kwa mkataba wa kandarasi wa EPC. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi aprili 2018.

Mradi wa BaraBara Kuu ya Umeme Afrika Mashari-
ki Kilomita 612 (Mradi wa Kuunganisha Ethio-
pia-Kenya)

Mradi wa kuunganisha Ethiopia-Kenya (unaofahamika pia kama mradi wa Barabara Kuu ya Umeme ya Afrika Mashariki) utaiunganisha Kenya na mifu-

mo ya nishati ya umeme ya nchi ya Ethiopia. Unahusisha ujenzi wa laini ya kilomita 612 ya nguvu ya 500kV HVDC yenye uwezo wa kusafirisha umeme kwa njia ya Bipolar kutoka Ethiopia hadi kituo kidogo cha umeme cha Suswa na vituo vya kubadilisha umeme katika pande zote mbili. Laini hii itakuwa na uwezo wa kusafirisha Megawati 2000 kati ya nchi hizi mbili. Pindi utakapokamilika, utawezesha Kenya na Ethiopia pamoja na nchi nyingine jirani kuchangamkia safu mbalimbali za vyanzo vya nishati vinavyopatikana katika uzalishaji wa umeme.

Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AFD na Serikali ya Kenya kwa gharama za KSh. Bilioni 63.2. Katika mwaka tukiokuwa chini ya ukaguzi, mchakato kwa ajili ya miundo na mchoro wa uhandisi unaendelea. Laini hii ya kusambaza umeme inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba 2018 ilhali kituo cha kubadilisha umeme kitakamilika mwezi Machi 2019.

Mradi wa Kuunganisha Kenya – Tanzania (Kilomita 93, 400kV)

Mradi huu ni sehemu ya upande wa Kenya ya Laini ya kuunganisha nchi jirani ya kilomita 2,000 inayohusisha nchi za Kenya–Tanzania–Zambia ambao utaunganisha Mtandao wa Umeme wa nchi za Kusini mwa Afrika huku ikitoa fursa za biashara ya nishati ya umeme kati ya Mtandao wa Umeme wa nchi za Afrika Mashariki (EAPP) na Mtandao wa Umeme wa nchi za Kusini Mwa Afrika (SAPP). Unahusisha ujenzi wa laini ya kusambaza umeme



Vifaa kwenye kituo
cha umeme





Laini ya kusambaza umeme ya Ethiopia- Kenya

>>>>>>>>>

ya kilomita 93 yenye uwezo wa 400kV na saketi mbili kutoka Isinya nchini Kenya hadi Namanga mpakani na Tanzania. Katika mwaka tuliokuwa chini ya ukaguzi, mchakato wa kutafuta washauri wa ukandarasi na mkandarasi wa “EPC contractor” ulikamilika. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2018.

IV. Miradi ya Upatikanaji Umeme

Miradi ya kikundi hiki ipo kwenye mpango wa taifa wa Programu ya Kupanua Upatikanaji wa Nishati ya Umeme na lengo kuu la miradi hii ni kuongeza upatikanaji wa umeme na kukabiliana na changamoto ya kupata na kujiunga na huduma ya umeme. Miradi chini ya programu hii ni kama ifuatavyo:

(a) Miradi ya Kupanua Mfumo wa Kusambaza Umeme

Laini ya Nanyuki – Isiolo (Kilomita 96, 132kV)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya kilomita 96 yenye uwezo wa 132kV na saketi moja na nguvu ya kusafirisha umeme wa Megawati 73 kutoka kituo kidogo cha umeme cha Nanyuki hadi Isiolo na

Meru. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo kidogo kipya cha umeme hapo Isiolo na upanuzi wa vituo vidogo vya umeme vya Nanyuki na Meru. Ukamilifu wa jumla wa mradi huu umefikia asilimia 98.2. Kipande cha laini ya Meru-Isiolo (km 26) na vituo vidogo vya umeme vilikamilika na kuanza kutumika. Ujenzi wa kipande cha Nanyuki-Isiolo umesimma kutokana na masuala ya ufinyu wa njia.

Laini ya Sondu–Homa Bay–Ndhiwa-Awendo

Laini ya kilomita 100 yenye uwezo wa 132kV na saketi moja kutoka Sondu hadi Homa Bay na Awendo yenye nguvu ya kusafirisha umeme wa Megawati 72 na inahusisha kituo kidogo kipya cha umeme cha Homa Bay na upanuzi wa vituo vigo-gu vya umeme vya Sondu na Awendo. Unalenga kuimarisha mtandao uliopo wa nishati ya umeme katika Nyaza ya kusini na kuongeza upatikanaji wa umeme. Mradi huu unakadiriwa kugharimu KSh. Bilioni 2.3 kwa ufadhili wa Benki ya KBC ya Ubegiji na Serikali ya Kenya.

Katika mwaka tuliokuwa chini ya ukaguzi, uchunguzi wa udongo kwa laini za usambazaji pamoja na vituo vya umeme ulikamilika, mchoro wa uhan-



disi na ujenzi vinaendelea. Hata hivyo, kukosekana kwa fedha kutoka hazina kulichelewesha upigaji hatua wa mradi huu. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2018.

(b) Mpango ya Upanuzi wa Nishati ya Umeme Nchini (KEEP)

KEEP ni mpango wa Benki ya Dunia na Serikali ya Kenya unaojumuisha miradi ya kuzalisha, kusambaza na kufikisha umeme. Kipengele cha kusambaza kinajumuisha laini za kusambaza umeme za kilomita 354 na uwezo wa 132kV pamoja na vituo vidogo husika vya umeme. Malengo ya jumla ya mradi huu yapo katika sehemu mbili (i) kuongeza uwezo, ufanisi na ubora wa ugavi wa umeme (ii) kupanua upatikanaji wa umeme sehemu za mijini, maeneo ya vitongoji vya miji na maeneo ya vijijini. Unafadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Kenya kwa ghrarama ya KSh. Bilioni 6.4. Mradi huu unahusisha laini zifuatazo:-

Laini ya Kindaruma – Mwingi – Garissa (Kilomita 250, 132kV)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya 132kV na saketi moja kutoka Kindaruma kupitia Mwingi hadi Garissa pamoja na vituo vidogo vipya vya umeme vya Mwingi na Garissa na ujenzi wa upanuzi wa kituo kidogo cha umeme kilichopo Kindaruma. Pindi utakapokamilika, utaboresha ubora wa ugavi huko Mwingi na kupelekea kuhamishwa kwa majenereta aghali ya dizeli yasiyo katika gridi huko Garissa pamoja na kusafirisha nishati ya umeme kutoka miradi pendekezwa ya Feed in Tariff katika meneo ya kaskazini mwa Kenya. Mradi huu ulikamilika mwezi Aprili 2016 na kuwashwa na kufunguliwa na Mheshimiwa Raisi mwezi Mei 2016.

Laini ya Eldoret – Kitale (Kilomita 60, 132kV)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya kusambaza umeme yenye uwezo wa 132kV na saketi moja kutoka Eldoret hadi Kitale, ujenzi wa kituo kidogo kippya cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV

Wafanyikazi
wa KETRACO
wakifunzwa
kuhusu SAP

>>>>>>>>>>



huko Kitale na outgoing bay kwenye kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132kv cha Eldoret. Mradi ulikamilika mwezi Juni 2016.

Laini ya Kisii – Awendo (Kilomita 44, 132kV)

Mradi huu unahusisha ujenzi wa laini ya kusambaza umeme ya 132kV na saketi moja kutoka Kisii hadi Awendo, ujenzi wa kituo kidogo kipya cha umeme huko Awendo na outgoing bay kwenye kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132kV cha Kisii. Ujenzi wa laini na hatua za awali za kukifungua kituo kidogo cha umeme bado unaendelea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2017.

(c) Programu ya Kuboresha Mfumo wa Kusambaza Nishati ya Umeme Kenya (KPTSIP)

Kampuni inatekeleza pia mradi unaoitwa Programu ya Kuboresha Mfumo wa Kusambaza Nishati ya Umeme Kenya (KPTSIP), unaojumuisha laini sita zilizoainishwa hapo chini zenye jumla ya urefu wa kilomita 431 na vituo vidogo vya umeme 14. Programu ya KPTSIP inafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) na Serikali ya Kenya kwa jumla ya gharama ya KSh. Bilioni 8.1

Laini hizi zitaongeza upatikanaji wa umeme kati ka maeneo ya kaunti za Baringo, Laikipia, Narok, Bomet, Kitui, Makueni, Embu na maeneo ya jirani. Upatikanaji wa ugavi wa uhakika wa umeme utayabadilisha maeneo haya kuwa vivutio vya viwanda vya mazao ya kilimo na viwanda vinginevyo na hivyo kusaidia kuunga mkono mamlaka za kiserikali za ukanda huu. Miradi hii inajumuisha ujenzi wa laini zifuatazo na vituo vidogo husika vya :

i. Laini ya Lessos – Kabarnet (Kilomita 65, 132kV), kituo kidogo kipya cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Kabarnet na outgoing bay kwenye kituo kidogo cha umeme cha Lessos; Vituo vidogo vya umeme vimekamiliika na kwa sasa vipo katika mchakato wa majaribio ya kuvifungua, ujenzi wa laini nao pia unaendelea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2016.

ii. Laini ya Nanyuki – Nyahururu [Rumuruti] (Kilomita 79, 132kV), kituo kidogo kipya cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Nyahururu na upanuzi wa kituo kidogo kipya cha umeme cha Nanyuki; Vituo vidogo vya umeme vimekamiliika na vipo katika mchakato wa majaribio ya kuvifungua, ujenzi wa laini ya kusambaza umeme umesimama kutokana na masuala ya ufinyu wa njia na KDF. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili 2017.

iii. Laini ya Olkaria – Narok (Kilomita 68, 132kV), kituo kidogo kipya cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Narok na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Olkaria; Kituo kidogo cha umeme kimekamiliika kwa asilimia 100 na kipo kwenye mchakato wa majaribio ya kufungua. Ujenzi wa laini ya kusambaza umeme unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili 2017.

iv. Laini ya Sotik – Bomet (Kilomita 33, 132kV) na kituo kidogo kipya cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Bomet na Sotik; Mradi huu ulikamilika na kuanza kufanya kazi mwezi Agosti 2016;

v. Laini ya Mwingi – Kitui – Wote – Sultan Hamud (Kilomita 153, 132kV), vituo vidogo vipya vya umeme vyenye uwezo wa 132/33kV huko Kitui, Wote na Sultan Hamud, na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Mwingi; ujenzi wa vituo vidogo vya umeme umekamilika kwa asilimia 100 na vipo kwenye mchakato wa majaribio ya kuvifungua. Ujenzi wa laini ya kusambaza umeme unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili 2017.

vi. Laini ya Ishiara – Kieni (Kilomita 33, 132kV), kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Kieni na switchgear huko Ishiara. Ujenzi wa vituo vidogo vya umeme umekamilika kwa asilimia 100 na mchakato wa kufanya majaribio ya kuvifungua unaendelea. Mradi huu ulikamilika mwezi Septemba 2016.

Miradi inayofadhiliwa na Benki ya EXIM ya India na Serikali ya Kenya:

Jumla ya urefu wa laini za kusambaza umeme ni kilomita 243 na ujenzi wake unafadhiliwa na Benki ya Exim ya India na Serikali ya Kenya kwa Dola za Marekani Milioni 62. Miradi hii inatarajiwa kuanza mwaka 2016/2017.

a. Laini ya Turkwel – Ortum – Kitale

Laini ya kilomita 90 yenye uwezo wa 220kV na saketi moja kutoka mtambo wa nishati ya umeme wa Turkwel hadi Ortum na Kitale; ina uwezo wa kusafirisha nguvu ya umeme ya Megawati 250. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa vituo vidogo vipya vya umeme huko Ortum na Kitale na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Turkwel pamoja na kupeleka ugavi wa umeme kwenye kiwanda pen-dekezwa cha saruji huko Ortum. Ujenzi wa laini ya kusambaza umeme na vituo vidogo vya umeme unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2017.

b. Laini ya Machakos – Konza – Kajiado – Namanga

Laini ya kilomita 153 yenye uwezo wa 132kV na saketi moja kutoka Machakos hadi Konza, Kajiado na Namanga ina uwezo wa kusafirisha nguvu ya umeme ya Megawati 73. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa vituo vidogo vinne (4) vya umeme huko Machakos, Konza, Kajiado na Namanga. Utai-marisha mitandao ya umeme iliyopo maeneo hayo pamoja na kuongeza upatikanaji wa umeme katika kaunti za Machakos, Makeni na Kajiado na maeneo ya jirani. Ujenzi wa laini ya kusambaza umeme na vituo vidogo vya umeme unaendelea. Ujenzi wa kituo kidogo cha umeme cha Konza umekamilika na kinafanya kazi na mchakato wa kukifungua kituo kidogo cha umeme cha Machakos unaendelea. Kipande cha Machakos - Konza kitafunguliwa mwezi Oktoba 2016 huku kipande cha Kajiado-Namanga kitafunguliwa mwezi Aprili 2017.

V. Miradi inayohitaji ufadhili

KETRACO imebainisha miradi ya ziada ya laini za kusambaza umeme inayohitaji ufadhili. Baadi ya miradi inategemewa kusafirisha umeme unaozalishwa, kuimarisha mfumo wa umeme huku minigine itawezesha upanuzi wa gridi kwenye maeneo ya mbali na hivyo kuongeza upatikanaji wa umeme hata huko. Miradi hii inajumuisha ifuatayo:

- i. Laini ya Silali – Rongai (Kilomita 150, 400kV)
- ii. Laini ya Menengai – Rongai (Kilomita 25, 400kV)
- iii. Laini ya Isinya – Nairobi Mashariki (Kilomita 110, 400kV)
- iv. Laini ya Meru – Maua (Kilomita 50, 132kV) na kituo kidogo cha umeme cha Maua chenye uwezo wa 132/33kV 7.5MVA yenye makadirio ya gharama ya KSh. Bilioni 1.4;
- v. Laini ya Rumuruti – Marahal (Kilomita 148, 132kV) na saketi moja na kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV 7.5MVA huko Maralal na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Nyahururu na mradi huu unakadiriwa kugharimu KSh. Bilioni 2.1;
- vi. Laini ya Awendo – Isabania (Kilomita 50, 132kV) na saketi moja na kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 133/33kV 23MVA huko Isabania na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Awendo, mradi unakadiriwa kugharimu KSh. Bilioni 1.4;
- vii. Laini ya Garsen – Hola – Bura – Garissa (Kilomita 240, 220kV) na saketi moja na vituo vidogo vya umeme huko Hola na Bura na upanuzi wa vituo vidogo vya umeme vya Garsen na Garissa. Makadirio ya gharama ni KSh Bilioni 4.2;
- viii. Laini ya Galu – Lunga Lunga (Kilomita 60, 132kV) na saketi moja na kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV 23MVA huko Lunga Lunga na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Galu. Makadirio ya gharama ni KSh Bilioni 1.6;





Picha ya usiku ya kituo kidogo cha umeme cha Suswa

- ix. Laini ya Ishiara – Chogoria (Kilomita 40, 132kV) na saketi moja na kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Chogoria na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Ishiara. Makadirio ya gharama ni KSh. Bilioni 1.3;
- x. Laini ya Garissa – Habaswen – Wajir (Kilomita 330, 220kV) yenye saketi moja pamoja na kituo kidogo cha umeme huko Wajir na Habaswen na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Garissa. Makadirio ya gharama ni KShs Bilioni 7.3;
- xi. Laini ya Voi – Taveta (Kilomita 107, 132kV) yenye saketi moja na kituo kidogo cha umeme chenye uwezo wa 132/33kV huko Taveta. Makadirio ya gharama ni KSh. Bilioni 2.6;
- xii. Laini ya Rabai – Bamburi – Kilifi (Kilomita 60, 132kV) yenye saketi mbili kutoka Rabai hadi Bamburi, 132 kV na saketi moja hadi Kilifi, 132kV huko Rabai, na vituo vidogo viwili vya umeme Bamburi na Mtwapa. Makadirio ya gharama ni KSh Bilioni 2.7;
- xiii. Laini ya Suswa – Ngong (Kilomita 40, 220kV) na mradi unakadiriwa kugharimu KSh Bilioni 1.9;
- xiv. Laini ya Kabarnet – Nyahururu [Rumuruti] (Kilomita 111, 132kV) na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme na unakadiriwa kugharimu KSh Bilioni 1.9;
- xv. Laini ya Narok – Bomet (Kilomita 88, 132kV) na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme unakadiriwa kugharimu KSh. Bilioni 1.7.
- xvi. Laini ya Kisumu – Kakamega – Musaga (Kilomita 70, 220kV) ya saketi mbili na kituo kidogo cha umeme huko Kakamega.
- xvii. Laini ya Webuye – Kimilili – Kitale (Kilomita 73, 132kV), ujenzi wa vituo vidogo vya umeme huko Webuye na Kimilili na upanuzi wa kituo kidogo cha umeme cha Kitale.



- xviii. Laini ya kusambaza umeme ya Kakamega – Kaimosi (Kilomita 25, 132KV) na ujenzi wa vituo vidogo vya umeme huko Kaimosi.
- xix. Laini ya kusambaza umeme ya Sotik – Kilgoris (Kilomita 48, 132kv) na kituo kidogo kipa cha umeme huko Kilgoris.
- xx. Laini ya Isinya – Konza (Kilomita 38, 400kv) yenye saketi mbili na kituo kidogo cha umeme huko Konza ambayo itauunganisha Mji wa kiteknolojia wa Konza (ICT city) katika gridi ya 400kv na vituo vya kuzalisha umeme huko Olkaria, Menengai na ng'ambo;
- xxi. Laini ya Gilgil – Thika – Nairobi Mashariki (Kilomita 205, 400kv) yenye saketi mbili na vituo vidogo vya umeme huko Longonot, Thika, Kangumdo na Konza itakayokamilisha laini ya Mzunguko wa Naironi yenye uwezo wa 400kv ambayo bado inajengwa kwa kutoa hakikisho la kuaminika la usalama la N-1.
- xxii. Laini ya Kamburu – Embu [Kutus] – Thika (Kilomita 196, 220kv) na upanuzi wa vituo vidogo vya umeme huko Kamburu, Embu, Kiganjo na Thika;
- xxiii. Laini ya Kitui – Mutomo – Kibwezi (Kilomita 144, 132kv) na ujenzi wa vituo vidogo vya umeme huko Kitui, Mutomo na Kibwezi;
- xxiv. Laini ya Ngong – Magadi (Kilomita 84, 132kv) na kituo kidogo cha umeme Magadi;
- xxv. Ujenzi wa kituo kidogo cha umeme Uplands, chenye uwezo wa 132/33 kV;
- xxvi. Laini ya Galu T off – Likoni (Kilomita 15, 132kv) na ujenzi wa kituo kidogo cha umeme huko Likoni;
- xxvii. Laini ya Rongai – Kilgoris (Kilomita 235, 400kv) pamoja na vituo vidogo vya umeme huko Rongai na Kilgoris na inatoa uwezekano wa kuunganika na Tanzania ili kukamilisha Mzunguko wa Ziwa Viktoria;
- xxviii. Laini ya Myanga – Busia (Kilomita 41, 132kv) na vituo vidogo vya umeme huko Myanga na Busia;
- xxix. Laini ya Rangala – Bondo – Ndigwa (Kilomita 72, 132kv) na ujenzi wa vituo vidogo vya umeme huko Bondo na Ndigwa;



Kuchimba kwa mashimo yakujenga mikingi ya umeme

<<<<<<<<<<



Wafanyikazi wa KETRACO
wakionyesha umoja wao
kwenye hafla ya kuwaleta
pamoja

>>>>>>>>>>



- xxx. Laini ya Homa Bay – Sindo (Kilomita 72, 132kV) na kituo kidogo cha umeme huko Sindo;
- xxxi. Laini ya Ndhiwa – Karungo (Kilomita 72, 132kV) na upanuzi wa vituo vidogo vya umeme vya Ndhiwa na Karungo;
- xxxii. Laini ya Kiambere – Maua – Isiolo (Kilomita 288, 220kV) na vituo vidogo vya umeme vyenye uwezo wa 220/132kV huko Maua na Isiolo;
- xxxiii. Laini ya Isiolo – Maralal (Kilomita 152, 220kV) kama mbadala kwa ajili ya kusafirisha umeme kutoka mitambo ijayo ya nishati ya upepo na jua;
- xxxiv. Laini ya Isiolo – Marsabit (Kilomita 306, 220kV) na upanuzi wa vituo vidogo vya umeme huko Isiolo na Marsabit;
- xxxv. Laini ya Loiyangalani – Marsabit (Kilomita 188, 400kV) pamoja na kituo kidogo cha umeme huko Marsabit ambacho kitaweze kutumia kikamilifu fursa ya kuzalisha umeme kupitia chanzo cha upepo huko kaskazini mwa Kenya;
- xxxvi. Laini ya Turkwel – Lodwar – Lokichogio (Kilomita 228, 220kV) na ujenzi wa vituo vidogo vya umeme huko Turkwel, Lodwar na Lokichogio.

Mafanikio mengine

Ili kutekeleza kikamilifu majukumu yake, kampuni inahitaji kuhakikisha inaweka mazingira hamasishi na wezeshi yanayosaidia utumiaji mkamilifu wa fursa za shirika letu. Ninayo furaha kuripoti kwamba pamoja na kuandaa Mpango Mkakati wetu wa 2015/16-2019/20, Kampuni iliweza kutekeleza programu nyinginezo katika nyanja mbalimbali za majukumu yake ya kazi kama vile kuboresha uwezo wa rasilimali watu, kuboresha miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT), mapitio na maboresho ya mifumo sahihi, sera, miundo na michakato kama ilivyoainishwa hapo chini. Suala hili limeiwezesha Kampuni kujiweka katika nafasi nzuri ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi na kuweza kujiandaa kuwasilisha mipango yake kwenye mnyororo wa ugavi wa umeme nchini Kenya.

Kuandaa Mpango Mkakati 2015/16-2019/20

Mwaka tuliokuwa chini ya ukaguzi ulikuwa mwanzo wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa awamu ya pili wa kampuni ya KETRACO. Baada ya kutekeleza kikamilifu Mpango Mkakati wake wa awamu ya kwanza, Kampuni iliandaa Mpango Mkakati mpya kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 – 2019/2020. Mpango Mkakati huu mpya umeainisha uelekeo wa kimkakati wa Kampuni kwa

kipindi cha miaka mitano ijayo na umesisitiza kuwekeza nguvu kwenye maendeleo ya miundombinu ya kusambaza umeme, kuitumia na kuifanyia marekebisha miundombinu hiyo, kusimamia nishati ya umeme na kuiwezesha biashara ya nishati ya umeme ya ndani ya nchi na ya kikanda.

Ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi na kuwa na mchango wake muhimu katika uchumi wa nchi na ukanda wa Afrika Mashariki, mkakati wa Kampuni umeegemezwwa kwenye nguzo sita zifuatazo za kimkakati, ambazo zinaunda maeneo muhimu ya kimatokeo: (i) Kuboresha na Kupanga Mifumo ya Kuzambaza Umeme; (ii) Kusimamia na Kushughulikia Mfumo wa Kusambaza Umeme; (iii) Mifumo ya Kiseru na Kisheria; (iv) Uendeleu na Uratibu wa Fedha; (v) Uwezo wa Shirika; na (vi) Kuwashirikisha Wadau.

Uzinduzi wa Mpango Mkakati wa awamu ya pili wa KETRACO tarehe 31 Machi 2016

Katika kipindi cha Mpango Mkakati huu KETRACO itajenga takribani kilomita 7,000 za laini za kusambaza umeme za msongo mkubwa wa umeme (132kV na zaidi) na vituo vidogo husika vya umeme, itaendelea kuimarisha uwezo wake katika kusimamia miradi na kuandaa programu za kuwashirikisha wadau ili kuhakikisha miradi yake inakamilika ndani ya muda, itajenga na kuimarisha uwezo wake wa kusimamia shughuli na matengenezo ya miundombinu ya kusambaza umeme, itajenga National Load Dispatch na Control Centre ifikapo 2018/19 na kujenga ofisi za kimkoa kwenye maeneo ya miradi muhimu nchini ikiwa ni miongoni mwa mipango mingine muhimu. Wakati huo huo, kampuni ilifanya mapitio ya muundo wake wa uongozi na kuanza utekelezaji wa suala hilo.

Kuendeleza Rasilimali Watu

Kampuni ilipiga hatua kubwa katika mchakato wake wa kuendeleza uwezo wa rasilimali watu kwa kiwango kizuri, kitu ambacho ni kigezo cha utendaji kazi wenye ufanisi unaohitajika ili kufikia lengo la kuwa kampuni ya kusambaza umeme yenye haki ya kimataifa. Kuhusiana na hili, Kampuni ilien-

delea kujitahidi kuwaongezea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapa mafunzo yanayopatikana hapa nyumbani na nchi za ng'ambo katika nyanja muhimu zilizobainika kutokana na kufanya tathmini ya uhitaji wa mafunzo. Wafanyakazi mbalimbali walihudhuria mafunzo muhimu ya kiufundi yanayotolewa sambamba na shughuli za kikazi chini ya miradi na vipengele vya mafunzo.

Ili kuwezesha kampuni kutekeleza majukumu yake ipasavyo, iliimarisha mchakato wa utafutaji wa wafanyakazi, uajiri, na ugawaji majukumu kwa wafanyakazi: wafanyakazi zaidi walijiunga na Kampuni katika mpango wa kudumu pamoja na mpango wa kimkataba na kupelekea kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi kufikia 355 hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Kampuni ilihakikisha anuwai katika usimamizi wa rasilimali watu na usawa wa kijinsia ulizingatiwa wakati wa kutafuta wafanyakazi wapya na kugawa majukumu ya kazi. Sera ya usawa wa kijinsia ilien-delea kutekelezwa na Sera ya Ukatili wa Kijinsia iliandaliwa.

Wafanyakazi pia walifundishwa kuhusu masuala ya kijinsia na kujilinda dhidi ya maaambukizi ya VVU na huduma zake. Aidha, sera ya usawa kwa watu wenye ulemavu iliandaliwa na watu wenye ulemavu walipewa fursa sawa wakati wa mchakato wa kutafuta wafanyakazi wapya.

Uendeshaji Biashara kwa njia ya Ufundi Mitambo

Kampuni iliendelea na utumiaji wa mitambo katika shughuli zake za kibiashara ili kuongeza ufanisi na thamani kwenye shughuli zake pamoja na huduma zinazotolewa. Ili kuandaa mfumo shirikishi wa usimamizi wa taarifa, kampuni ya INDRA Consultants ilipewa mkataba wa kuweka mfumo wa Upangaji na Matumizi ya Rasilimali za Kampuni (ERP). Awamu ya Kwanza ya mfumo wa SAP ERP ilianza kazi mwezi Januari 2016 na imeweza na kufanikisha mtiririko wa taarifa kati ya shughuli zote za kibiashara ndani ya Kampuni na kupelekea kupatikana kwa huduma zilizoboreshwa. Moduli



tano zilifungwa chini ya awamu ya kwanza ikiwa ni pamoja na (i) Usimamizi wa Vifaa, (ii) Mfumo wa Mradi, (iii) Fedha na Udhibiti, (iv) Usimamizi wa Mtaji Watu na Mfumo wa Ulipaji Mishahara, na (v) Usimamizi wa Fedha.

Kampuni bado ina dhamira ya kujenga na kuwekeza kwenye miundombinu ya hadhi ya kimataifa inayoendeshwa kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ili kukuza upelekeaji wa shughuli zake pamoja na huduma. Miradi ya laini za kusambaza umeme inayoendelea kujengwa imefungwa uwezo wa kubeba nyuzi aina ya Fibre (Optical Ground Wire - OPGW) ili kuwezesha matumizi ya mfumo wa mawasiliano ya ndani na kushirikishana takwimu ndani ya kampuni yaani Supervisory Control & Data Acquisition and Energy Management Systems (SCADA/EMS). Mradi wa kuongeza uwezo wa mtandao na upanuzi ulitekelezwa. Kampuni pia iliamisha kikamilifu na kujenga mtandao na miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kwenye ofisi yake mpya iliyopo KAWI Complex.

Usimamizi wa Utendaji

Usimamizi wa utendaji ni jambo muhimu kwenye shirika lolote lenye nia ya kukua na wakati tulipokuwa chini ya ukaguzi, Mafunzo ya Usimamizi wa Utendaji, Uundaji na Utekelezaji wa Vifaa Bora, washauri walimaliza kazi na wafanyakazi wote wa Kampuni walisaini mikataba ya utendaji kama sehemu ya Mfumo wa Kutathmini Utendaji. Aidha, utekelezaji wa Mikataba wa Utendaji kwa mwaka 2014/2015 ulifanyiwa tathmini na Serikali na Kampuni ilipata alama ya ujumla ya 2.9574, hivyo utendaji ulithaminishwa kuwa ni 'Vizuri Sana'.

Cheti cha ISO

Katika mwaka tuliokuwa chini ya ukaguzi, Ukaguzi wa Fedha ulitekelezwa na utumiaji wa shughuli za uendeshaji kupitia mitambo ya programu ya kuhakikisha utendakazi bora wa makampuni duniani inayojulikana kama ISO QMS, yaliendelea.

Kuwawezesha Vijana na Wanawake

Sambamba na Sera ya Serikali ya sasa ya kuwawezesha Vijana na Wanawake nchini, Kampuni ilikuwa mstari wa mbele katika jambo hilo.

Wanafunzi arobaini na nane (48) wa vyuo vikuu walipewa fursa ya kufanya kazi kwenye Kampuni kama industrial attachment. Zaidi, katika bajeti ya jumla ya manunuzi kwa mwaka ya KSh. Milioni 125 kwa ajili ya vifaa vya jumla ikiwa ni pamoja na vitu vya matumizi ya ofisini, takribani KSh. Milioni 39 zilipelekwa kwa vikundi/biashara zinazomilikiwa na vijana na wanawake pamoja na watu wenye ulemavu na kuandikishwa na Hazina ya Taifa.

Utunzaji wa Mazingira

Kulinda na kutunza mazingira ilibaki kuwa kipaumbele cha Kampuni na mipango kadhaa ilifanyika kuhusiana na lengo hili la kiungwana. Jumuiya pamoja na wafanyakazi walifundishwa kuhusu utunzaji wa mazingira. Ushirikiano na NEMA na KFS ulidumishwa wakati wa kufanya uthamini wa ESIA na uthamini wa njia kwa miradi yote mipya. Usimamizi wa ESMP na kaguzi za mazingira zilifanyika kwenye miradi inayojengwa na iliyokamilika kwa mtiririko huo.

Kuboresha Huduma kwa Wateja

Sambamba na maadili yetu ya msingi ya kumweka mteja kwanza, Kampuni inatambua kwamba kuboresha huduma kwa wateja ni jambo la muhimu ili kukamilisha majukumu yake ipasavyo. Mbali na wazalishaji na wasambazaji wa nishati ya umeme, ambao ni wateja wakuu, kampuni inawatendea kwa usawa wadau wengine wote kama wateja wa kibishara. Hivyo, Kampuni iliendelea na mchakato wa kutoa taarifa na kuwapa uelewa wateja kwa njia ya midahalo shirikishi kama vile vikao vya kuelimisha umma, kupanga na kushauri, kufungua kinywa na vyombo vya habari, mikutano ya kiuwekezaji na maonesho ya kibiashara. Kampuni iliendelea kuboresha mchakato wa kutoa zabuni/manunuzi, kuboresha sehemu ya mapokezi, kutoa mrejesho kwa wateja ndani ya muda na kukuza uwezo wa wafanyakazi katika nyanja ya mahusiano na wateja.

Ili kupima kiwango cha kuridhika kwa wateja wetu, Kampuni iliajiri kampuni ya nje ambayo ilifanya uthamini wa kuridhika kwa wateja (2015/16 exit survey), ambayo ilitoa ripoti ya jumla ya kuridhika kwa wateja kwa kiwango cha asilimia 78.2. Uthamini huo ilibainisha matakwa ya wateja na ulitoa mapendekezo ya maboresho.



Wajibu wa Shirika kwa Jamii (CSR)

Ikiongozwa na kanuni za kuwajibika kwa kampuni katika jamii, Kampuni inadunisha dhamira yake ya kushirikisha jumua mahalia kwenye maeneo yanayoathiriwa na mradi, umma wote, washirika wa kisékta na wadau wengine ikiwa na lengo la kujenga uaminifu kwao, ushirikiano na uhusiano wa kirafiki. Kwa msingi huu, KETRACO ilihakikisha kwamba miradi yote inatekelezwa kupitia mchakato wa kuwashirikisha washauri (consultative process) tangu hatua ya awali ya kuweka mipango ya mradi husika hadi kukamilika kwake. Zaidi, Kampuni ilihakikisha kwamba shughuli zake zilifanyika kwa kuzingatia taratibu za kitaalamu na kibinadamu ukizingatia kwamba ujenzi wa laini za kusambaza umeme unahusisha umiliki wa ardhi kwa ajili ya vituo vidogo vya umeme na upatikanaji wa njia kwa ajili ya laini. Suala hili linahusisha kulipa fidia na wakati mwingine kuwahamisha kimakazi watu walioathiriwa na Miradi (PAPs) na hitaji la kutekeleza mchakato huu kwa makubaliano ya pande zote mbili. Ikiongozwa na Sera yake ya Wajibu wa Shirika kwa Jamii (CSR) Kampuni ilishiriki kikamilifu kwenye vikao mbalimbali pamoja na wadau.

Shukrani

Ninachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhauti kwa Serikali, wabia wa kimaendeleo, washauri, wakandarasi, watu walioathiriwa na miradi yetu, uongozi wa Kampuni na wafanyakazi na wadau wetu wote, kwa ushirikiano na msaada wao unaoendelea hata hivi leo, katika kipindi cha mwaka 2015/2016. Hakuna mafaniko tuliyoyapata ambayo yangefanikiwa bila ya mchango kutoka kwa kila mmoja wenu. Kwa umoja na ushirikiano wenu unaoendelea hata hivi leo, Kampuni imeendelea kuweka mkazo katika kuwezesha huduma ya uga-vi wa nishati ya umeme iliyo bora, ya uhakika, na salama ili kuunga mkono ajenda ya kitaifa ya maendeleo.



FCPA. Fernandes Barasa
Mkurugenzi Mkuu
Machi 28 2017



Corporate Governance Statement

1. INTRODUCTION

KETRACO's Board of Directors and management strongly support the principles of good corporate governance, and are committed to building on the Company's strong reputation for integrity. The governance arrangements adopted by the Company are reflective of a high performing well governed organization.

This governance framework enables the Board and management to make well informed decisions, provide appropriate accountability and transparency, and establish the proper culture and behaviors. For KETRACO this is essential as it enhances our opportunities to achieve our objectives.

2. CORPORATE GOVERNANCE STATEMENT

This Corporate Governance Statement outlines the main corporate governance principles and practices obtaining during the 2015/2016 financial year and at the date of this statement. The Company's corporate governance practices are reviewed regularly and will continue to be developed and refined to meet the needs of the Company and taking account of best practice. KETRACO observed the following governance framework during the year under review.

(i) Board Manual and Committee Charter

KETRACO has put in place mechanisms for a corporate governance framework which is outlined in the Board Manual and Committee Charters approved by the previous Board.

The framework ensures separation of functions and duties of the Board and shareholders, the duties of the Board and Management, the duties of the Chairman and Managing Director, and responsibilities of individual directors and the Board as an entity.

(ii) MWONGOZO

The Government, through the State Corporations Advisory Committee and the Public Service Commission issued "MWONGOZO" The Code of Governance for State Corporations in January, 2015. It stated that this Code of Governance is a Government response to the need for effective utilization of public resources. The reforms are targeted at achieving improvement in public service delivery as part of the wider public reforms. The Government developed Mwongozo as a critical building block in entrenching principles and values of public service and best practices in corporate governance geared to address the challenges of governance in State Corporations.

The State Corporations Advisory Committee is expected to come up with a roadmap for all state corporations to implement the Code of Governance. The Directors of KETRACO attended a workshop organized by the State Corporations Advisory Committee late last year to sensitize the directors on the operationalization of MWONGOZO. KETRACO will review its Board and Committee Charters to align them to "MWONGOZO". All Directors have access to an electronic copy of the Code which was uploaded in the eBoard System for easy reference and perusal as per the Code's requirements.

(iii) KETRACO's Code of Conduct

The Code of Conduct applies to Directors, executives, management and employees, sets high standards for ethical behaviour and business practice beyond complying with the law and is based on guiding principles. The Code of Conduct also sets out the Company's policies in respect of ethical issues such as conflicts of interest, social accountability and fair dealing.



3. eBOARD SYSTEM

The Board of KETRACO has embraced technology to effectively and efficiently conduct its business. In this regard, the Board introduced an electronic system for conducting board meetings and other functions, eliminating paper work. All the members have undergone training to effectively interrogate and use the electronic system.

4. BOARD AND MANAGEMENT COMPOSITION, ROLES AND RESPONSIBILITIES

(i) Board Composition

The Memorandum & Articles of Association of the Company provide that the appointment and removal of Board shall be governed by the provisions of the State Corporations Act. The constitution of the Board is provided under the Memorandum & Articles of Association Section 3. The Board of Directors shall consist of: -

- a) A non-executive Chairman appointed by the President
- b) The Chief Executive appointed by the Cabinet Secretary for the time being responsible for Energy
- c) The Principal Secretary for the time being responsible for Energy or his representative
- d) The Cabinet Secretary in the Ministry for the time being responsible for Finance or his representative
- e) Five other members from the private sector appointed by the Minister for the time being responsible for Energy.

The current Board with nine (9) members is, therefore, properly constituted as provided above.

(ii) Board Roles and Responsibilities

KETRACO has put in place mechanisms for a corporate governance framework which is outlined in the Board Manual and Committee Charters.

The framework ensures separation of functions and duties of the Board and shareholders, the duties of the Board and Management, the duties of the Chairman and Managing Director, and responsibilities of individual directors and the Board as an entity.

The Company observed this governance framework during the year under review.

To assist the Board with carrying out its responsibilities, certain powers have been delegated to management, including the authority to undertake transactions and incur expenditure on behalf of the Board up to specified thresholds.

Management provides relevant information to the Board in a concise and timely manner to enable the Board to make informed decisions and effectively discharge their duties. The Board regularly monitors the flow of information it receives from management, and Directors may request additional information where necessary.



5. BOARD PERFORMANCE EVALUATION

